**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**

**MAWASILIANO NA UONGOZI WA SHULE.**

**Mkuu wa Shule 0757594915/0699827570**

**Makamu Mkuu wa Shule. 0687207777**

**MTAALUMA. 0787860748**

**Shule ya Sekondari KIKUNDE.**

**S.L.P. 69 SONGE – KILINDI, TANGA**

**Tarehe........................................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ________________________________________**
**S.L.P ______________________**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIKUNDE HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI MKOA WA TANGA MWAKA..................................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka.............................na atasoma tahasusi ya _______

Shule hii ipo Mkoa wa Tanga katika wilaya ya Kilindi,Shule ipo kijiji cha KIKUNDE kilometa 75 kutoka makao makuu ya Wilaya ya **KILINDI –SONGE**. Kwa Wanafunzi wanaotokea DAR ES - SALAAM. ARUSHA Na KILIMANJARO watapanda mabasi yanayoelekea MOROGORO-DODOMA Watashukia Gairo stendi ya Shabibi ambapo watapanda NOAH Za KIKUNDE mahali ilipo shule hii, Kwa wale wanaotokea Mikoa ya Nyanda za juu kusini,Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati watafika DODOMA na kupanda mabasi yanayopitia njia ya Gairo na kwenda Stendi ya Shabibi ambapo pia watapanda NOAH Za KIKUNDE na kushukia Katika Stand ya Kikunde ambapo kutoka stendi ya Kikunde Hadi shuleni Ni Umbali wa KM 1.5 Na Usafiri wa Bodaboda hadi shuleni unapatikana kwa Tsh.1000/= tu

Muhula wa Masomo unaanza tarehe..................., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe................................ **Mwisho wa kuripoti ni tarehe**…………………

## 2. <u>MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-</u>

### 2.1 SARE ZA SHULE KWA WAVULANA NA WASICHANA

i. Sare ya shule hii ni SURUALI 2 RANGI YA DARK BLUE Yenye **MARINDA MAWILI** kila upande na isiwe ya kubana (**upana iwe inch 15).** Mwanafunzi anapoandaa maandalizi ya kushona suruali ahahakikishe anaenda na maelekezo ya namna ya ushonaji wa suruali kwa fundi kama fomu hii inavyoelekeza. **Kinyume na hapo suruali hii haitapokelewa shuleni.**

**WASICHANA**
**Sketi 2 Rangi ya DARK BLUE ,Rinda Box mbele na nyuma,ivuke goti na kuishia karibu na kifundo Cha Mguu.Tafadhali Zingatia maelekezo.**

ii. Mashati 2 meupe yenye mikono mirefu na isiwe ya kubana**( TOMATO)**
iii. Sare ya Michezo ni Track suit ya kijivu na raba rangi yeyote;
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na visiwe buti;
v. Soksi jozi mbili nyeusi
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa Wavulana.
vii. Sweta 1 rangi ya Dark blue lenye Nembo ya Shule. Mwanafunzi anaruhusiwa kuja na koti jeusi zito la ziada lisilo kua na kofia kwa sababu ya Baridi pia liwe la staha na lisilovuka magoti nalisiwe na maandishi yeyote.
viii. Nguo za kushindia tisheti 2 nyeupe za round color na isiwe Tshirt aina ya form six na zisiwe na maandishi yoyote na suruali 2 nyeusi zisiwe za kubana.
WASICHANA.
Nguo za kushindia Ni tishert 2 nyeupe za Round collar isiwe T-shirt ya form six na sisiwe na maandishi yeyote na Sketi 2 nyeusi Rinda box mbele na nyuma ndefu zenye Staha.
ix. Tai 2 NYEUSI.

**NB: NI MARUFUKU KUJA NA TSHIRT YA AINA YOYOTE ILE YA MICHEZO AU YA NYUMBANI ZAIDI YA TSHIRT ZILIZOANISHWA HAPO JUU AMBAZO PIA ZITATUMIKA KATIKA MICHEZO.**

### 2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-

i. Madaftari 7 ya counterbook Quire 3 AU Quire 4;
ii. **Ream (A4)** (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo vya Futi mbili na nusu kwa Sita (2.5 *6 ft) na unene wa inch 4.

v. Mashuka Jozi 2 rangi ya light blue, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1 lenye mpini., mifagio 2 (soft brooms na squezer) na reki moja.Jembe,kwanja na soft broom vinapatikana karibu na mazingira ya shule,jembe na mpini 10,000,kwanja 5000 na soft broom 4000.
x. Aje na sanduku la bati kwaajili ya kutunzia vifaa vyake binafsi.

.

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | **Mchango wa Uendeshaji wa Shule** | **65,000/=** |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

MCHANGO WA UENDESHAJI WA SHULE (65,000/=) FEDHA ZILIPIWE KUPITIA AKAUNTI YA SHULE AMBAYO NI **NMB 42601100020** JINA LA AKAUNTI **KIKUNDE SECONDARY SCHOOL CAPITATION.**

MICHANGO MINGINE YOTE ITALIPIWA SHULENI KWA MUHASIBU.

**NB: Mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA inayofanya kazi au aje na fedha taslimu Tsh. 54,000/= kwa kila mwaka wa masomo kwa ajili ya kutengenezewa BIMA YA AFYA.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

NB: Mwanafunzi hatavumiliwa kwa kuchelewa kufika shule baada ya Likizo; ADHABU KALI itatolewa Kwa mwanafuzi atakaechelewa kuanzia siku moja ya kuwasilishuleni

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KIKUNDE SEKONDARI.**

**.......................................**

**JOSEPH CYPRIAN MROKI.**

**MKUU WA SHULE KIKUNDE SEC SCHOOL**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0757594915/0699827570**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0687207777**
- **Mwandamizi Taaluma 0687860748**
- **Mwandamizi Malezi na AFYA 0688506381**

**UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI KIKUNDE.**

**SEHEMU A** : ( Ijazwe na mwanafunzi)

Mimi (jina kamili la mwanafunzi)……………………………………………………………………………..

Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………………………………

Dini……………………………………………………………………………………………...

Kijiji…………………………………wilaya………………………mkoa…………………………..

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuuingia kidato cha tano shule ya sekondari KIKUNDE.Nathibitisha kuwa nitatii na kufuata sheria zote za shule kama zilivyoainishwa. Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatau matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiriki katika migomo wala vurugu zozote shuleni bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa shule ili matatizo yatafutiwe ufumbuzi pindi yanapotokea.

Saini……………………………………………………………

Tarehe………………………………….

**SEHEMU B** :(Ijazwe na mzazi)

Mimi jina kamili…………………………………………… Namba ya simu………………………………………….

Kijiji…………………………Wilaya……………………Mkoa……………………………………

Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mwanangu nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule.nitahakikisha mtoto anaenda shule muda uliopangwa nanitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.

Saini ya mzazi………………………………………………..

Tarehe………………………………….

NB**: NGUO ZA NYUMBANI PAMOJA NA SIMU HAVITARUHUSIWA KABISA SHULENI.**

**PRIME MINISTER'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**KIKUNDE SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS**

KIKUNDE **SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.BOX 69**
**SONGE – KILINDI**.
**Date**…………………….

**MEDICAL OFFICER, GOVERNMENT HOSPITAL**

………………………………………………………….

**NAME OF STUDENT**…………………………………………………..

Please examine the above-named student to ascertain his fitness for admission to pursue studies.

**MEDICAL OFFICER,**

(To be completed by a medical officer)

I have examined the above named with regard to:

**Skin……………………………………………………………………………………………**
**Eyes……………………………………………………………………………………………**
**Ears……………………………………………………………………………………………**
**Chest…………………………………………………………………………………………**
**Spleen…………………………………………………………………………………………**
**Abdomen……………………………………………………………………………………**
**Urine…………………………………………………………………………………………**
**Stool……………………………………………………………………………………………**
**Hemoglobin**
**(HB)…………………………………………………………………………………………**

**I consider that:**

1. He is of good health,free from infectious diseases,worms,bilharzias and fit to pursue studies
2. He is now fit to return to school after having been treated for…………………………

Name and Designation----------------------------------- Signature……………………………..

Date…………………………………………

Official Stamp.